



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

HALI YA UCHAGUZI KATIKA MAENEO
MBALIMBALI NCHINI

Dar es Salaam, 28 Oktoba, 2020

Kama tunavyofahamu leo kuanzia saa 01.00 asubuhi zoezi la upigaji kura limenza katika vituo mbalimbali vya kupigia kura.

Mpaka sasa zoezi la uchaguzi linaendelea vizuri licha ya kuwepo kwa kasoro ndogondogo katika baadhi ya maeneo hasa kwa wapiga kura ambao hawakufanikiwa kuhakiki taarifa mapema na kuweza kutambua vituo vya kupigia kura.

Nitumie fursa hii pia kutoa taarifa kuwa, kuna Kata nne ambazo hazijafanya Uchaguzi wa Madiwani. Kata tatu kati ya hizo ni kutokana na baadhi ya wagombea kufariki na Kata moja haijafanya Uchaguzi kutokana na kukosewa kwa karatasi za kura. Kata ambazo hazijafanya uchaguzi kutokana na wagombea kufariki ni:-

- Igumbilo katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa.
- Kisingia katika Halmashauri ya Wilaya Kilolo.
- Nyahanga katika Halmashauri ya Mji wa Kahama.

Kwa mujibu wa kifungu cha 51(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa serikali za Mitaa Sura ya 292 kikisomwa pamoja kanuni ya 33 ya kanuni za uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za Mwaka


2020, Tume itapanga tarehe nyingine ya uteuzi wa wagombea wa vyama ambavyo, wagombea wake wamefariki.

Aidha, Kata ya Kibosho Kati, iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Moshi haijafanya uchaguzi wa Diwani kutokana na kukosewa kwa karatasi za kura za Kata hiyo. Kwa mujibu wa Kifungu cha 48(1) (b) cha Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Tume itapanga tarehe nyingine ya uchaguzi kwa Kata hiyo.

Hata hivyo, tukumbuke kuwa katika Kata hizo uchaguzi wa Rais na Wabunge unaendelea kama ulivyopangwa.

Aidha, kuna taarifa zinazosambaa kwenye mitandao ya kijamii kuhusu kuwepo kwa masanduku na kura feki katika majimbo ya Kawē (Dar es Salaam), Pangani (Tanga) na Buhigwe (Kigoma). Taarifa za madai hayo ya jumla, na ambayo siyo rasmi, hayajadhibitishwa na hayaelezi ni vituo vipi vinahusika na matukio hayo. Vivyo hivyo, taarifa za madai hayo hazijawasilishwa rasmi kwenye Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Tume inawasihi wananchi kupuuza taarifa hizo ambazo sio rasmi na hazijadhibitishwa.

Tume inaendelea kufuatilia namna ambavyo zoezi la uchaguzi linavyoendelea nchi nzima, na itatoa taarifa kwa kadri itakavyowezekana. Nitumie nafasi hii pia kuwahimiza wapiga kura ambao hawajafika katika vituo vyao vya kupigia kura kufanya hivyo kabla ya saa 10.00 jioni ambao ni muda wa kufunga vituo.



Jaji R (Mst) Semistocles S. Kaijage

MWENYEKITI

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI